OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA

SHULE YA SEKONDARI MAFULALA,
S.L.P 453,
SUMBAWANGA

JINA LA MWANAFUNZI……

1. UTANGULIZI

Ninayofuraha kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Mafulala kwa mwaka 2021

Shule ya sekondari mafulala ipo kilomita 8 kaskazini mashariki mwa mji wa Sumbawanga kata ya mafulala ,shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti siku hiyo bila kuchelewa .Mwisho wa kuripoti ni tarehe 17/01/2021

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1 . SARE YA SHULE

Ili kuwa na sare moja kwa wanafunzi wote(uniformity) uongozi wa shule unaagiza kutafuta vitambaa halisi vya sare.

A. WAVULANA

i. Suruali mbili (moja rangi nyeusi na ya pili kijani jeshi) Suruali iwe ya heshima ,pana na sio mchinjo
ii. Mashati mawili meupe mikono mifupi
iii. Viatu vyeusi vyenye kisigino kifupi vya kufunga na kamba.
iv. Socks jozi 2 nyeupe
v. Sweta rangi ya zambarau
vi. Mkanda mweusi.

B. WASICHANA

a. Sketi mbili (Moja rangi nyeusi ya pili kijani jeshi zenye malinda) iwe ndefu yenye kufunika soksi ili kuepukana na adha ya upepo mkali uliopo ukanda huu.
b. Mashati mawili meupe mikono mifupi
c. Viatu vyeusi vyenye kisigino kifupi vya kufunga na kamba.
d. Socks jozi 2 nyeupe
e. Sweta rangi ya zambarau
f. Kwa waislamu hijabu rangi nyeupe.

2:2 VIFAA VYA DARASANI

Mwanafunzi aje na vifaa vya darasani (mathematical set,Counter book quire 2 ziwe kumi, rula, penseli, biki na mfuto,

2:3 VIFAA VYA MICHEZO

i. Raba rangi yoyote
ii. Bukta au truck suit dark blue
iii. T-shirt rangi ya kijivu.

2:4 VIFAA VYA USAFI

Mwanafunzi aje na vifaa vya usafi (ndoo ndogo ya lita kumi, jembe, na fagio ya chelewa).

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya **Elimu Na. 25 ya mwaka 1978** na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995.Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana na Elimu nchini chini ya **Ofisi ya Rais (TAMISEMI),**Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo;

i. Heshima kwa viongozi,walimu,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
iii. Kushiriki kwa makini katika kufanya maandalio ya jioni (preparations)
iv. Kuwahi katika kila shughuli na nyinginezo utakazopewa.
v. Kuwepo ndani ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix. Kutunza mali za umma.

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

i. Wizi
ii. Uasherati na ushoga
iii. Ubakaji
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vila uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kubeli na kadhalika.
v. Kupigana au kupiga
vi. Kudharau bendera ya Taifa.
vii. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
viii. Kuwa mjamzito/kupata mimba
ix. Kuoa au kuolewa
x. Kutoa mimba
xi. Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
xii. Kukataa adhabu kwa makusudi
xiii. Kuwa na simu ya mkononi

4:0 Mambo mengine yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi ni';

(a) **Medical examination form(Fomu ya uchunguzi wa Afya ya mwanafunzi)** mwanafunzi anatakiwa kupimwa katika ofisi ya Mganga Mkuu wa manispaa ya Sumbawanga na si sehemu nyingine,baada ya vipimo fomu ijazwe na kuwasilishwa shuleni,

(b) **Fomu ya maelezo Binafsi** kuhusu historia ya mwanafunzi

(c) **Fomu ya mzazi** kukiri kukubaliana na sheria ,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa shuleni.

Nakutakia maandalizi mema na karibu sana Mafulala Sekondari.

……

ONESMO .R. LYAPITA

MKUU WA SHULE.

SHULE YA SEKONDARI MAFULALA

HISTORIA YA MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi……
Jina la baba ……..
Jina la mama ……
Shule ya msingi aliyosoma ……
Kijiji atokacho …… kitongoji cha ……
Tarehe ya kuzaliwa ……..... Dini ……Dhehebu ……..
Kabila …….

UTHIBITISHO:

5.1 Ahadi ya Mwanafunzi

Mimi …… nakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha …… mwaka ……. Katika shule ya Sekondari Lukangao, na ninaahidi:-

i. Kuzingatia taratibu na kanuni zote za shule
ii. Kuweka bidii katika masomo yote
iii. Kushiriki katika shughuli za elimu ya kujitegemea
iv. Kuwa na nidhamu ya juu ndani na nje ya shule

Jina …….
Sahihi ……
Tarehe ……...

5.2 Ahadi ya Mzazi / Mlezi

Mimi …… mzazi / mlezi wa ……..
Naahidi kwamba:

i. Nitatimiza gharama za mwanangu kama nilivyoelekezwa
ii. Nitamhimiza mwanangu kuzingatia taratibu za shule pamoja na masomo
iii. Nakubaliana na kanuni na sheria zilizotolewa na serikali juu ya mwanafunzi (mwanangu)

Jina ……
Sahihi ……
Tarehe ……...